JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# FOMATI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

**IMETOLEWA NA:**

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
S.L.P 2624
DAR ES SALAAM
TANZANIA

**APRILI, 2025**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# FOMATI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE


**IMETOLEWA NA:**

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
S.L.P 2624
DAR ES SALAAM
TANZANIA


**APRILI, 2025**

Imechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam,
Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024.

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI.......................................................................................................iv

L01 KISWAHILI.....................................................................................1

L02 ENGLISH LANGUAGE .....................................................................5

L03 FRENCH LANGUAGE......................................................................8

L04 LUGHA YA KIARABU.....................................................................12

L05 LUGHA YA KICHINA.......................................................................15

A06 JIOGRAFIA NA MAZINGIRA: SANAA NA MICHEZO...............................19

A07 HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI ..................................................23

M08 HISABATI ....................................................................................27

S09 SAYANSI......................................................................................30

# DIBAJI

Kitabu cha fomati za Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kimeandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa kuzingatia matakwa ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 toleo la mwaka 2023 na Mtaala ulioboreshwa wa Elimu ya Msingi Darasa la III hadi la IV wa mwaka 2023 uliotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Kitabu hiki kimeandaliwa ili kukidhi malengo ya mtaala na mihutasari iliyoboreshwa ambayo ni; kukuza stadi za Kusoma, Kuandika, Kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kubuni na kutatua matatizo, kubaini na kukuza vipaji, stadi za kazi, michezo na sanaa, kukuza tabia ya kuthamini na kupenda kufanya kazi, kutambua na kutumia sayansi na teknolojia, kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia; na kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

Fomati za Upimaji zilizopo katika kitabu hiki zitaanza kutumika mwaka 2025. Masomo ya lazima yatakayopimwa ni Kiswahili, *English Language*, Jiografia na Mazigira; Sanaa na Michezo, Hisabati, Sayansi na Historia ya Tanzania na Maadili. Aidha, masomo chaguzi yatakuwa *French Language*, Lugha ya Kiarabu na Lugha ya Kichina.

Fomati hii imeandaliwa kwa kufuata muundo wa aya tano katika kila somo ambazo ni Utangulizi, Malengo ya Jumla, Umahiri Mkuu, Umahiri Mahususi na Muundo wa Upimaji. Vilevile, Jedwali la Utahini kwa kila somo limeambatanishwa mwisho mwa fomati ya kila somo husika kwa lengo la kuonesha asilimia ya uzito wa kila umahiri unaopimwa.

Baraza la Mitihani lina imani kuwa, fomati hii itawawezesha watunzi, warekebishaji na walimu kuandaa maswali ya upimaji yatakayowezesha kupata matokeo ya haki, halali na madhubuti. Aidha, kitabu hiki cha fomati kisitumike kwa vyovyote vile kama mbadala wa mihtasari ya masomo husika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika kuandaa kitabu hiki.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# L01 KISWAHILI

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii inatokana na Muhtasari wa mwaka 2023 wa somo la Kiswahili na itaanza kutumika mwaka 2025. Fomati hii imezingatia uboreshaji wa mitaala ya mwaka 2023 ambapo malengo yake ni pamoja na kubaini kiwango cha wanafunzi wa Darasa la Tatu na Darasa la Nne cha udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yao.

Upimaji katika Fomati hii utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji wa mwanafunzi ili kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Maboresho yamefanyika katika idadi ya vipengele vya maswali ambapo Upimaji wa somo hili utakuwa na maswali **matano (5)** yenye vipengele **30**.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji wa somo la Kiswahili unalenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika:

2.1 kukuza stadi za kusoma, kuandika na kuwasiliana kwa lugha fasaha;
2.2 kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Kiswahili;
2.3 kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo; na
2.4 kukuza stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa Kiswahili.

## 3.0 UMAHIRI MKUU

Upimaji unalenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika:

3.1 kuwasiliana katika miktadha mbalimbali;
3.2 kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma; na
3.3 kuwasilisha hoja kwa mazungumzo na kwa maandishi kulingana na muktadha.

## 4.0 UMAHIRI MAHUSUSI

Upimaji wa somo la Kiswahili unalenga kupima umahiri wa wanafunzi katika:

4.1 kutambua matamshi ya sauti mbalimbali katika silabi, maneno, sentensi na habari;
4.2 kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali;
4.3 kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali;
4.4 kuonesha stadi za kusikiliza na kuelewa;
4.5 kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu;
4.6 kuwasilisha hoja kwa njia ya mazungumzo katika miktadha mbalimbali;
4.7 kuandika matini mbalimbali;
4.8 kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali; na
4.9 kuonesha stadi za awali za ubunifu wa kazi mbalimbali za Kiswahili.

## 5.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

Upimaji wa somo la Kiswahili utakuwa na karatasi **moja (1)** na utafanyika kwa muda wa saa **1:00**. Wanafunzi wenye mahitaji maalum watafanya Upimaji kwa muda wa saa **1:10**. Upimaji utakuwa na sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali **matano (5)** yenye jumla ya vipengele **30**. Mwanafunzi atatakiwa kujibu maswali **yote** yenye jumla ya alama **50**.

### 5.1 SEHEMU A

Sehemu hii itakuwa na maswali **mawili (2)**. Swali la kwanza litakuwa la imla. Swali hilo litakuwa na sentensi **tano (5)**. Kila sentensi itakuwa na maneno **manne (4)**. Mwanafunzi atatakiwa kusikiliza sentensi zitakazosomwa na kuandika kwa usahihi katika sehemu iliyoachwa wazi. Kila neno litakuwa na alama **0½.** Swali la pili litakuwa la kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguo **A – D** na litakuwa na vipengele **kumi (10)**. Kila kipengele kitakuwa na **alama 01**. Hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya **alama 20**.

### 5.2 SEHEMU B

Sehemu hii itakuwa na maswali **mawili (2)** yenye vipengele **vitano (05)** kila moja. Swali la tatu litakuwa la kujaza nafasi iliyoachwa wazi. Swali la nne litakuwa la kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta maana ili kuunda kifungu cha habari kwa kuzipa herufi **A**, **B**, **C**, **D** na **E**. Kila kipengele kitakuwa na **alama mbili (2)**. Hivyo, sehemu hii itakuwa na jumla ya **alama 20**.

### 5.3 SEHEMU C

Hii sehemu itakuwa na swali **moja (1)** la ufahamu. Swali hili litakuwa la kuandika majibu mafupi kutoka katika kifungu cha habari/ushairi au hadithi na litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Kila kipengele kitakuwa na **alama mbili (2)**. Hivyo, sehemu hii itakuwa na jumla ya **alama 10**.

## 6.0 JEDWALI LA KUTAHINI KISWAHILI

Jedwali la Utahini lifuatalo linaonesha umahiri mahususi utakaopimwa, idadi ya vipengele vya maswali na asilimia ya uzito kwa kila umahiri.

| Na. | Umahiri Mahususi | Ngazi za Nyanja ya Utambuzi Zitakazopimwa | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | Idadi ya Vipengele kwa Umahiri | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri |
| 1 | Kutambua matamshi ya sauti mbalimbali katika silabi, maneno, sentensi na habari. | | | | | | | 2 | 6.8 |
| 2 | Kuonesha stadi za kusikiliza na kuelewa. | | | | | | | 3 | 10.2 |
| 3 | Kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali. | | | | | | | 10 | 33.3 |
| 4 | Kuandika matini mbalimbali. | | | | | | | 3 | 10.2 |
| 5 | Kuwasilisha hoja kwa njia ya mazungumzo katika miktadha mbalimbali. | | | | | | | 2 | 6.7 |

| Na. | Umahiri Mahususi | Ngazi za Nyanja ya Utambuzi Zitakazopimwa | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | Idadi ya Vipengele kwa Umahiri | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri |
| 6 | Kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu. | | | | | | | 3 | 10.2 |
| 7 | Kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali. | | | | | | | 2 | 6.7 |
| 8 | Kuonesha stadi za awali za ubunifu wa kazi mbalimbali za Kiswahili. | | | | | | | 2 | 6.4 |
| 9 | Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali. | | | | | | | 3 | 9.5 |
| **Idadi ya Vipengele** | | | | | | | | **30** | **100** |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ujuzi** | | | | | | | | | |

# L02 ENGLISH LANGUAGE

## 1.0 INTRODUCTION

This format is based on the 2023 English Language Syllabus for Primary Education and will be used effectively from 2025 onwards. It outlines the main and specific English Language competencies pupils should acquire in standards III and IV. Moreover, the format indicates what ought to be assessed in the subject.

The assessment will adhere to the criteria set in the pupils' learning activities for assessing the extent to which the pupils' have developed knowledge and skills and the ability to perform different activities using acquired skills. The assessment will consist of **six (6)** questions with **32** items from **five (5)** specific competencies derived from all **three (3)** main competencies in the 2023 syllabus.

## 2.0 GENERAL OBJECTIVES

The English Language assessment aims at testing the pupil's ability to:

2.1 develop reading and writing skills; and
2.2 master, appreciate, and use the English language.

## 3.0 MAIN COMPETENCIES

The assessment will measure the pupil's ability to:

3.1 demonstrate mastery of basic English language skills;
3.2 comprehend oral and written information; and
3.3 communicate effectively in different contexts.

## 4.0 SPECIFIC COMPETENCIES

The assessment will measure the pupil's ability to:

4.1 develop listening skills and demonstrate basic skills in creative writing;
4.2 develop phonemic awareness;
4.3 demonstrate knowledge of the basic features of spoken language;

4.4 use appropriate grammar and vocabulary both orally and in writing, relating words with objects in the environment and

4.5 produce short written messages and respond in a familiar communicative context.

## 5.0 ASSESSMENT RUBRIC

The English Language assessment will consist of **one (1)** paper to be completed in **1:00** hour. Pupils with special needs will take **1:10** hour. The paper will comprise three sections **A**, **B**, and **C** with **six (6)** questions and **32** items. Pupils will be required to answer all the questions, worth **50** marks.

### 5.1 SECTION A

This section will consist of **three (3)** questions. The first question will be on dictation. The question will consist of **five (5)** sentences each consist of **four (4)** words. Pupils will be required to listen attentively to the sentences read and write them correctly. Each word carrying **0½** marks. The second question will consist of **ten (10)** multiple-choice items. The pupil will choose the answer from options **A** to **D**. Each item will carry **one (01)** mark. The third question will be on filling in the gaps. This question will consist of **five (5)** items, weighing **two (2)** marks each. This section will carry **30** marks.

### 5.2 SECTION B

This section will have **two (2)** questions, 4 and 5. Question 4 will consist of **three (3)** items on jumbled letters. The pupil will arrange the letters to form words. Each item will carry **two (02)** marks. Question 5 will consist of **four (4)** filling-in-the-blank space items. The pupil should change words provided in the brackets into their correct form to complete a given short written message. Each item will carry **one (01)** mark. This section will weigh a total of **10** marks.

### 5.3 SECTION C

This section will comprise **one (1)** short answer question (Question 6). The pupil will be required to read and comprehend a passage and then respond to **five (5)** short-answer items. Each item will carry **two (2)** marks. The section will weigh **10** marks.

## 6.0 ENGLISH LANGUAGE TABLE OF SPECIFICATIONS

The following Table of Specifications presents specific competencies for assessment, the number of items and the percentage weight of each competency:

| S/N | Specific Competencles | Cognitive Levels to be Tested | | | | | | Number of Items per Competence | Percentage Weighting per Competence |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Remembering | Understanding | Applying | Analysing | Evaluating | Creating | | |
| 1 | Develop listening skills and demonstrate basic skills in creative writing. | | | | | | | 5 | 17 |
| 2 | Develop phonemic awareness. | | | | | | | 5 | 16 |
| 3 | Demonstrating knowledge of the basic features of spoken language. | | | | | | | 7 | 23 |
| 4 | Use appropriate grammar and vocabulary both orally and in writing, relating words with objects in the environment. | | | | | | | 11 | 36 |
| 5 | Produce short written messages and respond in a familiar communicative context. | | | | | | | 4 | 8 |
| **Number of Items** | | | | | | | | **32** | **100** |
| **Total Percentage Weight of Items per Cognitive Level** | | | | | | | | | |

# L03 FRENCH LANGUAGE

## 1.0 INTRODUCTION

This format is based on the 2023 French Language Syllabus for Primary Education and will be used effectively from 2025. The format considers the main and specific competencies the pupils should acquire in each class from standard III to VI.

This format consists of **six (6)** questions with a total of **30** items designed to assess all eight specific competencies derived from **three (3)** main competencies. The format will enable a pupil to demonstrate the ability to cope with the development of Science and Technology in the contemporary world and, thus, build foundational competence for higher classes in other levels of primary education.

## 2.0 GENERAL OBJECTIVES

The French Language assessment aims at testing the pupil's ability to:

2.1 develop the four language skills of speaking, listening, reading and writing;

2.2 master, appreciate and use the French Language;

2.3 recognise and use science and technology in learning and real life; and

2.4 learn and recognise other people's cultures.

## 3.0 MAIN COMPETENCIES

The assessment will focus on the pupil's ability to:

3.1 demonstrate mastery of basic French language skills;

3.2 comprehend oral and written information; and

3.3 communicate effectively in different contexts.

## 4.0 4.0 SPECIFIC COMPETENCIES

The assessment will measure the pupil's competencies in:

4.1 listening and understanding simple information;

4.2 demonstrating knowledge of basic spoken French features;

4.3 associating words with objects in the environment;
4.4 developing phonemic awareness and pronunciation of French letters;
4.5 mastering simple grammar and vocabulary;
4.6 speaking in different contexts, using appropriate grammar and vocabulary;
4.7 responding appropriately to a familiar communicative context; and
4.8 reading and comprehending simple texts.

## 5.0 ASSESSMENT RUBRIC

The French Language assessment will consist of **one (1)** paper to be completed in **1:00** hour. Pupils with special needs will take **1:10** hour. It will comprise three sections **A**, **B**, and **C** with **six (6)** questions and **30** items. Pupils will be required to answer all the questions accounting for **50** marks.

### 5.1 SECTION A

This section will consist of **two (2)** questions. The first question will consist of multiple-choice items or dictation. The multiple-choice question will require pupils to choose the correct answer from options **A - D**. Each item will carry **one (01)** mark. The second question will be on filling in the gaps using given sound parts to make meaningful words. This question will consist of **five (5)** items with **one (01)** mark each. This section will carry a total of **10** marks.

### 5.2 SECTION B

This section will have **three (3)** questions. The third question will be on dialogue. A pupil must complete a dialogue by writing the missing sentences or words in the spaces provided. This question will consist of **six (6)** items carrying **two (02)** marks each. The fourth question will consist of **five (5)** items on jumbled words or sentences; a pupil must arrange mixed words or sentences. Each item will carry **two (02)** marks. The fifth question will be on filling in the gaps.

This question will consist of **four (4)** items carrying **two (02)** marks each. This section will weigh a total of **30** marks.

### 5.3 SECTION C

This section will comprise **one (1)** short answer question (Question 6) on reading and comprehending the written information and respond to **five (5)** short answer items. Each item will carry **two (2)** marks. The section will weigh a total of **10** marks.

## 6.0 FRENCH LANGUAGE TABLE OF SPECIFICATIONS

The following Table of Specifications presents specific competencies for assessment, the number of items and the percentage weight for each competency.

| **S/N** | **Specific Competencies** | **Cognitive Levels to be Tested** | | | | | | **Number of Items per Competence** | **Percentage Weighting per Competency** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Remembering** | **Understanding** | **Applying** | **Analysing** | **Evaluating** | **Creating** | | |
| 1 | Listening and understanding of simple information. | | | | | | | 2 | 6.6 |
| 2 | Demonstrating knowledge of the basic spoken French features. | | | | | | | 3 | 10.1 |
| 3 | Associating words with objects in the environment. | | | | | | | 5 | 16.7 |
| 4 | Developing phonemic awareness and pronunciation of French letters. | | | | | | | 2 | 6.6 |
| 5 | Mastering simple grammar and vocabulary. | | | | | | | 5 | 16.7 |
| 6 | Speaking in different contexts, using appropriate grammar and vocabulary. | | | | | | | 6 | 20.0 |
| 7 | Responding appropriately to a familiar communicative context. | | | | | | | 2 | 6.6 |

| S/N | Specific Competencies | Cognitive Levels to be Tested | | | | | | Number of Items per Competence | Percentage Weighting per Competency |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Remembering | Understanding | Applying | Analysing | Evaluating | Creating | | |
| 8 | Reading and comprehending simple texts. | | | | | | | 5 | 16.7 |
| **Number of Items** | | | | | | | | **30** | |
| **Total Percentage Weight of items per Cognitive level** | | | | | | | | | **100** |

## L04 LUGHA YA KIARABU

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya upimaji wa somo la Lugha ya Kiarabu inatokana na Muhtasari wa somo la Lugha ya Kiarabu uliotolewa mwaka 2023 na itaanza kutumika mwaka 2025. Fomati hii imejikita katika kupima kiwango cha ujifunzaji wa wanafunzi wa Darasa la Tatu na Darasa la Nne katika somo la Lugha ya Kiarabu.

Upimaji huu una lengo la kupima jinsi mwanafunzi anavyoweza kutumia ujuzi alioupata katika kutatua matatizo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia katika jamii ili kujiletea maendeleo binafsi na Taifa kwa jumla. Upimaji wa somo hili utakuwa na maswali **sita (6)** yenye jumla ya vipengele **30**.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji wa somo la Lugha ya Kiarabu unalenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika:

2.1 kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa Lugha ya Kiarabu; na
2.2 kutumia lugha ya Kiarabu kwa urahisi kulingana na mahitaji ya mawasiliano katika miktadha mbalimbali.

## 3.0 UMAHIRI MKUU

Upimaji unalenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika:

3.1 kumudu stadi za msingi za Lugha ya Kiarabu;
3.2 kuonesha uelewa wa taarifa katika mazungumzo na maandishi; na
3.3 kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali.

## 4.0 UMAHIRI MAHUSUSI:

Upimaji wa somo la Lugha ya Kiarabu unalenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika;

4.1 kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya herufi za Kiarabu na uandishi wake;
4.2 kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira;

4.3 kumudu sarufi na msamiati sahili;
4.4 kusikiliza na kuelewa taarifa;
4.5 Kusikiliza na kuelewa taarifa zilizotolewa kwa mdomo;
4.6 kusoma na kuelewa matini sahili;
4.7 kuonesha mwitiko sahihi katika muktadha wa kimawasiliano unaofahamika; na
4.8 kuonesha uelewa wa sifa za msingi za lugha ya mazungumzo na maandishi.

## 5.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

Karatasi ya Upimaji wa Lugha ya Kiarabu itakuwa na sehemu **A** na **B**. Upimaji utakuwa na maswali **sita (06)** yenye jumla ya vipengele **30**. Muda wa kufanya upimaji utakuwa saa **1:00**. Wanafunzi wenye mahitaji maalumu watafanya Upimaji kwa muda wa saa **1:10**. Upimaji huu utakuwa na jumla ya alama **50**.

### 5.1 SEHEMU A

Sehemu hii itakuwa na maswali **matatu** (**3**). Swali la kwanza, la pili na la tatu. Swali la kwanza litakuwa la kuchagua kati ya chaguzi **A – D** au la imla. Swali hili litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Swali la pili litakuwa la kuoanisha na litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Wanafunzi watatakiwa kuoanisha vipengele katika Orodha **A** na majibu yake kutoka Orodha **B**. Kila kipengele katika maswali haya kitakuwa na alama **moja (1)**. Swali la tatu litakuwa la kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku/mabano na litakuwa na vipengele **vitano** (**5**). Kila kipengele katika swali hili kitakuwa na alama **mbili (2)**. Hivyo kufanya sehemu hii kuwa na alama **20**.

### 5.2 SEHEMU B

Sehemu hii itakuwa na maswali **matatu (3)**. Swali la 4, la 5 na la 6. Maswali haya yatakuwa ya majibu mafupi (kupanga herufi au maneno/kujaza nafasi zilizo wazi/maswali ya majibu mafupi/ mazungumzo (*dialogue*) au kusoma kifungu cha habari kitakachoambatana na majibu mafupi). Kila swali

litakuwa na vipengele **vitano** (**5**) na kila kipengele kitakuwa na alama **mbili** (**02**). Hivyo sehemu hii itakuwa na alama **30**.

## 6.0 JEDWALI LA KUTAHINI LUGHA YA KIARABU

Jedwali la Utahini lifuatalo linaonesha umahiri mahususi, idadi ya vipengele vya maswali na asilimia ya uzito kwa kila umahiri.

| Na. | Umahiri Mahususi | Ngazi za Nyanja za Utambuzi Zitakazopimwa | | | | | | Idadi ya Vipengele | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | | |
| 1 | Kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya herufi za Kiarabu na uandishi wake. | | | | | | | 5 | 17.14 |
| 2 | Kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira. | | | | | | | 5 | 17.14 |
| 3 | Kumudu sarufi na msamiati sahili. | | | | | | | 5 | 15.71 |
| 4 | Kusikiliza na kuelewa taarifa. | | | | | | | 3 | 8.57 |
| 5 | Kusikiliza na kuelewa taarifa zilizotolewa kwa mdomo. | | | | | | | 3 | 8.57 |
| 6 | Kusoma na kuelewa matini sahili. | | | | | | | 2 | 7.14 |
| 7 | Kuonesha mwitiko sahihi katika muktadha wa kimawasiliano unaofahamika. | | | | | | | 3 | 11.43 |
| 8 | Kuonesha uelewa wa sifa za msingi za lugha ya mazungumzo na maandishi. | | | | | | | 4 | 14.29 |
| **Idadi ya Vipengele** | | | | | | | | **30** | |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ujuzi** | | | | | | | | | **100** |

# L05 LUGHA YA KICHINA

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya upimaji wa somo la Lugha ya Kichina inatokana na Muhtasari wa somo la Lugha ya Kichina wa mwaka 2023 na itaanza kutumika mwaka 2025. Fomati hii imezingatia malengo ya Upimaji wa Elimu Msingi Darasa la Tatu na la Nne ambayo ni pamoja na kufuatilia kiwango cha ujifunzaji wa wanafunzi wa Darasa la Tatu na Darasa la Nne katika somo la Lugha ya Kichina.

Upimaji huu una lengo la kumjengea mwanafunzi udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake. Upimaji wa somo hili utakuwa na maswali **sita (6)** yenye jumla ya vipengele **30**.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji wa somo la Lugha ya Kichina unalenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika:

2.1 kukuza stadi za Kusoma, Kuandika, Kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha;
2.2 kufahamu, kutumia na kuthamini Lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha moja ya kigeni;
2.3 kuthamini na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, Umoja wa Kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;
2.4 kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;
2.5 kukuza maadili, uadilifu, na kuheshimu tofauti za imani;
2.6 kubaini na kukuza vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa;
2.7 kukuza tabia ya kuthamini na kupenda kufanya kazi;
2.8 kutambua na kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na katika maisha ya kila siku;
2.9 kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na
2.10 kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 3.0 UMAHIRI MKUU

Upimaji unalenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika:

3.1 kumudu stadi za msingi za Lugha ya Kichina;
3.2 kuonesha uelewa wa taarifa katika mazunguzo na maandishi; na
3.3 kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali.

## 4.0 UMAHIRI MAHUSUSI

Upimaji wa somo la Lugha ya Kichina unalenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika:

4.1 kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya awali, mwisho, toni, na *hanzi*;
4.2 kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira;
4.3 kumudu sarufi na msamiati sahili;
4.4 kuonesha mwitiko sahihi katika muktadha wa kimawasiliano unaofahamika;
4.5 kuonesha uelewa wa sifa za msingi za Lugha ya mazungumzo na maandishi;
4.6 kusikiliza na kuelewa taarifa;
4.7 kusoma na kuelewa matini sahili; na
4.8 kuzungumza katika miktadha mbalimbali kwa kutumia sarufi na msamiati mwafaka.

## 5.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

Upimaji wa somo la Lugha ya Kichina utafanyika kwa muda wa saa **1:00**. Wanafunzi wenye mahitaji maalum watafanya Upimaji kwa muda wa saa **1:10**. Upimaji utakuwa na sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **sita (6)** na vipengele **30**. Mwanafunzi atatakiwa kujibu maswali **yote** yenye jumla ya alama **hamsini (50)**.

### 5.1 SEHEMU A

Sehemu hii itakuwa na maswali **matatu (3)**. Swali la kwanza litakuwa la kuchagua jibu sahihi kati ya machaguo **A – D** au la imla na litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Swali la pili litakuwa la kuoanisha dhana mbalimbali. Swali hilo litakuwa

na vipengele **vitano (5)**. Wanafunzi watatakiwa kuoanisha vipengele katika Orodha **A** na majibu yake kutoka Orodha **B**. Swali la kwanza na la pili kila kipengele kitakuwa na alama **1** na kufanya jumla ya alama **10**. Swali la tatu litakuwa la kuchagua na kujaza nafasi iliyoachwa wazi. Swali hilo litakuwa na alama **10**, kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)**, hivyo, sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **20**.

### 5.2 SEHEMU B

Sehemu hii itakuwa na maswali **matatu (3)**. Swali la nne litakuwa la kujaza nafasi zilizoachwa wazi, ambalo litakuwa na vipengele **vinne (4)**. Swali la tano na la sita yatakuwa ya majibu mafupi, ambapo swali la tano litakuwa na vipengele **vitano (5)** na swali la sita litakuwa na vipengele **sita (6)** ambapo kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)**. Hivyo, sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **30**.

## 6.0 JEDWALI LA KUTAHINI LUGHA YA KICHINA

Jedwali la Utahini lifuatalo linaonesha umahiri Mahususi utakaopimwa, idadi ya vipengele vya maswali na asilimia ya uzito kwa kila umahiri.

| **Na.** | **Umahiri Mahususi** | **Ngazi za Nyanja ya Utambuzi Zitakazopimwa** | | | | | | **Idadi ya Vipengele** | **Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Kukumbuka** | **Kuelewa** | **Kutumia** | **Kuchambua** | **Kutathmini** | **Kuunda** | | |
| 1 | Kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya awali, mwisho, toni, na *hanzi* | | | | | | | 8 | 27.9 |
| 2 | Kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira. | | | | | | | 7 | 23.6 |
| 3 | Kumudu sarufi na msamiati sahili | | | | | | | 5 | 17.1 |

| Na. | Umahiri Mahususi | Ngazi za Nyanja ya Utambuzi Zitakazopimwa | | | | | | Idadi ya Vipengele | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | | |
| 4 | Kuonesha mwitiko sahihi katika muktadha wa kimawasiliano unaofahamika. | | | | | | | 2 | 7.1 |
| 5 | Kuonesha uelewa wa sifa za msingi za Lugha ya mazungumzo na maandishi. | | | | | | | 3 | 7.1 |
| 6 | Kusikiliza na kuelewa taarifa. | | | | | | | 2 | 7.1 |
| 7 | Kusoma na kuelewa matini sahili. | | | | | | | 2 | 7.1 |
| 8 | Kuzungumza katika miktadha mbalimbali kwa kutumia sarufi na msamiati mwafaka. | | | | | | | 1 | 2.8 |
| **Idadi ya Vipengele** | | | | | | | | **30** | |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ujuzi** | | | | | | | | | **100** |

# A06 JIOGRAFIA NA MAZINGIRA: SANAA NA MICHEZO

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii inatokana na mihtasari miwili ya mwaka 2023 ya somo la Jiografia na Mazingira na Sanaa na Michezo na itaanza kutumika kuanzia mwaka 2025. Fomati imezingatia maboresho ya mitaala ya mwaka 2023 ambapo malengo yake ni pamoja na kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku.

Upimaji utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji wa mwanafunzi ili kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Upimaji wa somo hili utakuwa na maswali **nane (8)** yenye jumla ya vipengele **30**.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji wa somo la Jiografia na Mazingira: Sanaa na Michezo unalenga kupima uwezo wa wanafunzi katika:

2.1 kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;
2.2 kukuza tabia ya kuthamini na kupenda kufanya kazi;
2.3 kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka;
2.4 kuchangamana katika mazingira jumuishi; na
2.5 kutumia vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa katika miktadha mbalimbali.

## 3.0 UMAHIRI MKUU

Upimaji wa somo la Jiografia na Mazingira: Sanaa na Michezo unalenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika:

3.1 kumudu stadi za awali za ramani na mfumo jua;
3.2 kumudu stadi za awali za sura ya nchi na rasilimali zilizopo;

3.3 kumudu misingi ya kutunza mazingira;
3.4 kubuni kazi za sanaa;
3.5 kuimarisha afya, stadi na ushindani; na
3.6 kumudu kazi za sanaa na michezo.

## 4.0 UMAHIRI MAHUSUSI

Upimaji wa somo la Jiografia na Mazingira: Sanaa na Michezo unalenga kupima umahiri wa wanafunzi katika:

4.1 kutumia ramani katika maisha ya kila siku;
4.2 kuonesha uelewa wa awali wa sura ya nchi;
4.3 kuonesha uelewa wa awali wa elimu ya kutunza mazingira;
4.4 kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji;
4.5 kuchora picha;
4.6 kufinyanga maumbo mbalimbali;
4.7 kumudu mazoezi ya viungo;
4.8 kucheza michezo ya asili;
4.9 kucheza michezo ya kisasa; na
4.10 kumudu stadi ya maonesho ya kazi za sanaa na michezo.

## 5.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

Upimaji wa somo la Jiografia na Mazingira: Sanaa na Michezo utakuwa na karatasi moja yenye jumla ya maswali **nane (8)** yenye vipengele **30**. Muda wa kufanya upimaji utakuwa saa **1:30**. Aidha, wanafunzi wenye mahitaji maalumu watafanya upimaji kwa muda wa saa **1:45**. Upimaji utakuwa na sehemu **A** na **B**. Sehemu ya **A** itahusu **Jiografia na Mazingira** na sehemu ya **B** itahusu **Sanaa na Michezo**. Jumla ya alama zitakuwa **hamsini (50)**.

### 5.1 SEHEMU A: JIOGRAFIA NA MAZINGIRA

Sehemu hii itakuwa na maswali **manne (4)** yenye jumla ya vipengele **16**. Mwanafunzi atatakiwa kujibu maswali **yote**. Swali la kwanza litakuwa la kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo **A - D** na litakuwa na vipengele **sita (6)** vyenye alama **moja (1)** kila kimoja. Swali la pili, tatu na nne yatakuwa ya majibu mafupi. Swali la pili litakuwa la kuchagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku na litakuwa na vipengele **vinne (4)**, swali la tatu litakuwa na vipengele **viwili (2)** vya kuandika majibu mafupi na swali la nne

litakuwa la kutafsiri picha/michoro/ramani na litakuwa na vipengele **vinne (4)**. Kila kipengele katika swali la pili hadi la nne kitakuwa na alama **mbili (2)**. Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **26**.

### 5.2 SEHEMU B: SANAA NA MICHEZO

Sehemu hii itakuwa na maswali **manne (4)** yenye jumla ya vipengele **14**. Mwanafunzi atatakiwa kujibu maswali **yote**. Swali la kwanza litakuwa la kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo **A - D** na litakuwa na vipengele **vinne (4)** vyenye alama **moja (1)** kila kimoja. Swali la pili, tatu na nne yatakuwa ya majibu mafupi. Swali la pili litakuwa la kuchagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku na litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Swali la tatu litakuwa la kuandika majibu mafupi na litakuwa na vipengele **viwili (2)** na swali la nne litakuwa la kutafsiri picha/michoro na litakuwa na vipengele **vitatu (3)**. Kila kipengele katika swali la pili hadi la nne kitakuwa na alama **mbili (2)**. Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **24**.

## 6.0 JEDWALI LA KUTAHINI JIOGRAFIA NA MAZINGIRA: SANAA NA MICHEZO

Jedwali la utahini lifuatalo linaonesha umahiri mahususi utakaopimwa, idadi ya vipengele na asilimia ya uzito kwa kila umahiri.

| **Na.** | **Umahiri Mahususi** | **Ngazi za Nyanja ya Utambuzi Zitakazopimwa** | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Kukumbuka** | **Kuelewa** | **Kutumia** | **Kuchambua** | **Kutathmini** | **Kuunda** | **Idadi ya vipengele** | **Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri mahususi** |
| 1 | Kutumia ramani katika maisha ya kila siku. | | | | | | | 10 | 33 |
| 2 | Kuonesha uelewa wa awali wa sura ya nchi. | | | | | | | 2 | 7 |
| 3 | Kuonesha uelewa wa awali wa elimu ya | | | | | | | 4 | 13 |

| Na. | Umahiri Mahususi | Ngazi za Nyanja ya Utambuzi Zitakazopimwa | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | Idadi ya vipengele | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri mahususi |
| | kutunza mazingira. | | | | | | | | |
| 4 | Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji. | | | | | | | 2 | 7 |
| 5 | Kuchora picha. | | | | | | | 2 | 7 |
| 6 | Kufinyanga maumbo mbalimbali. | | | | | | | 2 | 7 |
| 7 | Kumudu mazoezi ya viungo. | | | | | | | 2 | 7 |
| 8 | Kucheza michezo ya asili. | | | | | | | 2 | 7 |
| 9 | Kucheza michezo ya kisasa. | | | | | | | 1 | 2 |
| 10 | Kumudu stadi ya maonesho ya kazi za sanaa na michezo. | | | | | | | 3 | 10 |
| **Idadi ya Vipengele** | | | | | | | | **30** | **100** |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ujuzi** | | | | | | | | | |

## A07 HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya somo la Historia ya Tanzania na Maadii inatokana na muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili uliotolewa mwaka 2023 na itaanza kutumika mwaka 2025. Fomati hii imezingatia maboresho ya mitaala ya mwaka 2023 ambapo malengo yake ni pamoja na kuwa na wahitimu wenye maarifa na ujuzi utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku.

Upimaji katika Fomati hii utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji wa mwanafunzi ili kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Upimaji wa somo hili utakuwa na maswali **sita (6)** yenye jumla ya vipengele **35**.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji wa Historia ya Tanzania na Maadili unalenga kupima uwezo wa wanafunzi katika:

2.1 kuonesha, kuthamini na kuheshimu utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;
2.2 kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;
2.3 kuonesha uadilifu na kuheshimu tofauti za Imani;
2.4 kuthamini na kupenda kufanya kazi;
2.5 kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na
2.6 kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 3.0 UMAHIRI MKUU

Upimaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili unalenga kubaini umahiri wa mwanafunzi katika:

3.1 kulinda historia ya Tanzania, urithi na maadili ya taifa;
3.2 kumudu historia ya Tanzania na maadili kabla ya ukoloni; na
3.3 kumudu historia ya ujenzi wa taifa na maadili katika kipindi cha 1961-1966.

## 4.0 UMAHIRI MAHUSUSI

Upimaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili unalenga kupima umahiri wa wanafunzi katika:

4.1 kumudu dhana ya historia ya Tanzania, urithi na maadili;
4.2 kumudu maarifa ya jamii yanayomzunguka;
4.3 kutumia maarifa na ujuzi wa jamii inayomzunguka kusimulia asili, urithi na maadili ya jamii husika;
4.4 kutathmini ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi;
4.5 kueleza mifumo mbalimbali ya utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni;
4.6 kueleza maendeleo ya jamii za Kitanzania na maadili yake kabla ya ukoloni; na
4.7 kutumia alama za taifa kama utambulisho wa Tanzania.

## 5.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

Upimaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili utakuwa na karatasi **moja (1)** na utafanyika kwa muda wa saa **1:30**. Wanafunzi wenye mahitaji maalum utafanyika kwa muda wa saa **1:45**. Upimaji utakuwa na sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali **sita (6)** na vipengele **35**. Wanafunzi watatakiwa kujibu maswali **yote** katika kila sehemu. Jumla ya alama zitakuwa **50**.

### 5.1 SEHEMU A

Sehemu hii itakuwa na maswali **matatu (03)**. Swali la kwanza litakuwa la kuchagua jibu sahihi kati ya machaguo **A - D** lenye vipengele **kumi (10)**. Swali la pili litakuwa la kuoanisha dhana mbalimbali na litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Wanafunzi watatakiwa kuoanisha vipengele katika Orodha **A** na majibu yake kutoka Orodha **B**. Swali la tatu litakuwa la kuchagua jibu sahihi katika mabano/kisanduku na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi na litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Kila kipengele kitakuwa na alama **moja (01)**, hivyo kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa **20**.

### 5.2 SEHEMU B

Sehemu hii itakuwa na maswali **mawili (02)** ya majibu mafupi. Swali la nne litakuwa la vielelezo na litakuwa na vipengele **vinne (04)** na swali la tano litakuwa la picha au ramani na litakuwa na vipengele **vitano (05).** Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (02)**, hivyo kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa **18**.

### 5.3 SEHEMU C

Sehemu hii itakuwa na swali **moja (01)** la ufahamu/kupanga sentensi ili kuleta mantiki na litakuwa na vipengele **sita (06)**. Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (02)**. Hivyo sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **12**.

## 6.0 JEDWALI LA KUTAHINI HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

Jedwali la Utahini lifuatalo linaonesha umahiri mahususi utakaopimwa, idadi ya vipengele vya maswali na asilimia ya uzito kwa kila umahiri.

| **Na.** | **Umahiri Mahususi** | **Ngazi za Nyanja ya Utambuzi Zitakazopimwa** | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Kukumbuka** | **Kuelewa** | **Kutumia** | **Kuchambua** | **Kutathmini** | **Kuunda** | **Idadi ya vipengele kwa Umahiri** | **Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri** |
| 1 | Kumudu dhana ya historia ya Tanzania, urithi na maadili. | | | | | | | 2 | 3.23 |
| 2 | Kumudu maarifa ya jamii inayomzunguka. | | | | | | | 5 | 16.13 |
| 3 | Kutumia maarifa na ujuzi wa jamii inayomzunguka kusimulia asili, urithi, na maadili ya jamii husika. | | | | | | | 5 | 17.74 |

| Na. | Umahiri Mahususi | Ngazi za Nyanja ya Utambuzi Zitakazopimwa | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kukumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | Idadi ya vipengele kwa Umahiri | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri |
| 4 | Kutathmini ushirikiano baina ya jamii za kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii. | | | | | | | 4 | 9.67 |
| 5 | Kueleza mifumo mbalimbali ya utunzaji na ukuzaji wa maadili ya Jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. | | | | | | | 7 | 18.06 |
| 6 | Kueleza maendeleo ya jamii za kitanzania na maadili yake kabla ya ukoloni. | | | | | | | 10 | 31.94 |
| 7 | Kutumia Alama za Taifa kama Utambulisho wa Tanzania. | | | | | | | 2 | 3.23 |
| **Idadi ya Vipengele** | | | | | | | | **35** | **100** |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ujuzi** | | | | | | | | | |

# M08 HISABATI

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii inatokana na muhtasari wa Elimu ya Msingi wa mwaka 2023 wa somo la Hisabati na itaanza kutumika mwaka 2025. Fomati imezingatia uboreshaji wa mitaala ya mwaka 2023 ambapo malengo yake ni pamoja na kufuatilia kiwango cha ujifunzaji wa wanafunzi wa Darasa la III na Darasa la IV katika somo la Hisabati ili kumjengea mwanafunzi uwezo wa kuchunguza, kubuni, kushirikiana na kutatua matatizo katika mazingira yake.

Upimaji katika Fomati hii utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji wa mwanafunzi ili kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Upimaji wa somo hili utakuwa na maswali **sita (6)** yenye jumla ya vipengele **25**.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Malengo ya upimaji ni kupima uwezo wa mwanafunzi katika:

2.1 kukuza stadi za Kusoma, Kuandika, Kuhesabu na kuwasiliana kwa ufasaha;
2.2 kufikiri kimantiki, kubuni na kutatua matatizo;
2.3 kujijengea ari ya kupenda kutumia maarifa na mantiki za stadi za Hisabati kwa ajili ya maendeleo ya Jamii; na
2.4 kutambua na kutumia Hisabati katika kujifunza na katika maisha ya kila siku.

## 3.0 UMAHIRI MKUU

Upimaji wa somo la Hisabati unalenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika:

3.1 kumudu misingi ya awali ya kihisabati; na
3.2 kumudu matumizi ya stadi za kihisabati.

## 4.0 UMAHIRI MAHUSUSI

Upimaji utapima uwezo wa mwanafunzi katika:

4.1 kuonesha uelewa wa dhana ya namba;
4.2 kuonesha uelewa wa matendo ya namba;
4.3 kuonesha uelewa wa vipimo;
4.4 kuonesha uelewa wa awali wa stadi za maumbo;
4.5 kuonesha uelewa wa stadi za awali za namba;
4.6 kuonesha uelewa wa hesabu za muda; na
4.7 kuonesha uelewa wa hesabu za fedha.

## 5.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

Karatasi ya upimaji wa somo la Hisabati itakuwa na sehemu mbili, **A** na **B** na itakuwa na jumla ya maswali **sita (6)** yenye jumla ya vipengele **25**. Wanafunzi watatakiwa kujibu maswali yote. Jumla ya alama katika upimaji huu zitakuwa **hamsini (50)**. Muda wa kufanya maswali ya upimaji ni saa **1:30**. Aidha, wanafunzi wenye mahitaji maalumu watafanya upimaji kwa muda wa saa **2:00**.

### 5.1 SEHEMU A

Sehemu hii itakuwa na maswali **manne (4)** ya majibu mafupi yenye jumla ya vipengele **18**. Mwanafunzi atatakiwa kufanya matendo ya Kihisabati. Swali la kwanza litakuwa na vipengele **sita (6)**, la pili vipengele **vitano (5)**, la tatu litakuwa na vipengele **vitatu (3)** na la nne vipengele **vinne (4)**. Kila kipengele kitakuwa na uzito wa alama **mbili (2)**, hivyo kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa **36**.

### 5.2 SEHEMU B

Sehemu hii itakuwa na maswali **mawili (2)** ya maumbo na vipimo yenye jumla ya vipengele **saba (7)**. Swali la tano litakuwa na vipengele **vitatu (3)** na la sita litakuwa na vipengele **vinne (4)**. Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (02),** hivyo, jumla ya alama katika sehemu hii itakuwa **14**.

## 6.0 JEDWALI LA KUTAHINI HISABATI

Jedwali la Utahini lifuatalo linaonesha umahiri mahususi utakaopimwa, idadi ya vipengele vya maswali na asilimia ya uzito kwa kila umahiri.

| Na. | Umahiri Mahususi | Ngazi za Nyanja ya Utambuzi Zitakazopimwa | | | | | | Idadi ya Vipengele kwa Umahiri | Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kumbuka | Kuelewa | Kutumia | Kuchambua | Kutathmini | Kuunda | | |
| 1 | Kuonesha uelewa wa dhana ya namba. | | | | | | | 3 | 12.0 |
| 2 | Kuonesha uelewa wa matendo ya namba. | | | | | | | 3 | 12.0 |
| 3 | Kuonesha uelewa wa hesabu za vipimo. | | | | | | | 3 | 12.0 |
| 4 | Kuonesha uelewa wa awali wa stadi za maumbo. | | | | | | | 4 | 16.0 |
| 5 | Kuonesha uelewa wa stadi za awali za namba. | | | | | | | 5 | 20.0 |
| 6 | Kuonesha uelewa wa hesabu za muda. | | | | | | | 4 | 16.0 |
| 7 | Kuonesha uelewa wa hesabu za fedha. | | | | | | | 3 | 12.0 |
| **Idadi ya Vipengele** | | | | | | | | **25** | **100** |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ujuzi** | | | | | | | | | |

# S09 SAYANSI

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya somo la Sayansi imeandaliwa kutokana na Muhtasari wa somo la Sayansi wa mwaka 2023 na itaanza kutumika mwaka 2025. Fomati hii imezingatia malengo ya Upimaji wa Elimu ya Msingi Darasa la III - IV ikiwa ni pamoja na kubainisha kiwango cha ujifunzaji wa wanafunzi wa Darasa la IV katika somo la Sayansi.

Upimaji katika Fomati hii utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji wa mwanafunzi ili kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Upimaji wa somo hili utakuwa na maswali **sita (6)** yenye vipengele **30**.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji wa somo la Sayansi unalenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika:

2.1 kukuza uelewa na kutumia maarifa, stadi na kuwa na mwelekeo wa kisayansi na kiteknolojia;

2.2 kujenga uwezo wa kutumia Sayansi na Teknolojia katika kutatua matatizo katika maisha ya kila siku; na

2.3 kukuza ustadi wa kutumia vifaa mbalimbali vya Teknolojia katika ujifunzaji.

## 3.0 UMAHIRI MKUU

Upimaji unalenga kupima ujuzi na utendaji wa mwanafunzi katika:

3.1 kumudu nadharia za kisayansi;

3.2 kumudu stadi za awali za kisayansi;

3.3 kumudu matumizi ya TEHAMA; na

3.4 kubuni programu sahili za kompyuta.

## 4.0 UMAHIRI MAHUSUSI

Upimaji wa somo la Sayansi unalenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika:

4.1 kuonesha uelewa wa nadharia za kisayansi;
4.2 kufanya uchunguzi sahili wa kisayansi;
4.3 kuonesha uelewa wa aina za nishati na matumizi yake;
4.4 kufanya majaribio sahili ya kisayansi;
4.5 kutumia TEHAMA katika ujifunzaji; na
4.6 kubuni programu sahili za kompyuta.

## 5.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

Upimaji wa somo la Sayansi utakuwa karatasi **moja (1)** na utafanyika kwa muda wa saa **1:30**. Wanafunzi wenye mahitaji maalumu utafanyika kwa muda wa saa **1:45**. Upimaji utakuwa na sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **matano (5)** yenye vipengele **25**. Wanafunzi watatakiwa kujibu maswali **yote** katika kila sehemu. Jumla ya alama zitakuwa **50**.

### 5.1 SEHEMU A

Sehemu hii itakuwa na maswali **matatu (3)** yenye jumla ya vipengele **16**. Swali la kwanza litakuwa la kuchagua jibu sahihi na mwanafunzi atatakiwa kuchagua jibu sahihi kati ya machaguo **A – D** na litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Swali la pili litakuwa la kuoanisha na litakuwa na vipengele **vitano (5)**. Wanafunzi watatakiwa kuoanisha vipengele katika Safu **A** na majibu yake kutoka Safu **B**. Swali la tatu litakuwa la kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu kutoka katika kisanduku na litakuwa na vipengele **sita (6)**. Kila kipengele kitakuwa na uzito wa alama **moja (1)** kwa swali la kwanza na la pili na alama **mbili (2)** kwa swali la tatu, hivyo kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa **22**.

### 5.2 SEHEMU B

Sehemu hii itakuwa na maswali **matatu (3**) yenye jumla ya vipengele **14**. Swali la nne litakuwa la kupanga kanuni,

dhana au hatua za kisayansi ili kuleta mtiririko wenye mantiki. Swali hili litakuwa na vipengele **sita (6).** Swali la tano litakuwa la majibu mafupi ya kutafsiri picha au vielelezo na litakuwa na vipengele **sita (6).** Swali la sita litakuwa la majibu mafupi na litakuwa na vipengele **viwili (2)**. Kila kipengele kitakuwa na alama **mbili (2)**, hivyo kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa **28**.

## 6.0 JEDWALI LA KUTAHINI SAYANSI

Jedwali la Utahini lifuatalo linaonesha umahiri mahususi utakaopimwa, idadi ya vipengele vya maswali na asilimia ya uzito kwa kila umahiri.

| **Na.** | **Umahiri Mahususi** | **Ngazi za Nyanja ya Utambuzi Zitakazopimwa** | | | | | | **Idadi ya Vipengele kwa Umahiri** | **Asilimia ya uzito kwa kila Umahiri** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Kukumbuka** | **Kuelewa** | **Kutumia** | **Kuchambua** | **Kutathmini** | **Kuunda** | | |
| 1 | Kuonesha uelewa wa nadharia za Kisayansi. | | | | | | | 5 | 18.0 |
| 2 | Kufanya uchunguzi sahili wa kisayansi. | | | | | | | 6 | 19.0 |
| 3 | Kuonesha uelewa wa aina za nishati na matumizi yake. | | | | | | | 6 | 19.0 |
| 4 | Kufanya majaribio sahili ya kisayansi. | | | | | | | 5 | 18.0 |
| 5 | Kutumia TEHAMA katika ujifunzaji. | | | | | | | 6 | 19.0 |
| 6 | Kubuni programu sahili za kompyuta | | | | | | | 2 | 7.0 |
| **Idadi ya Vipengele** | | | | | | | | **30** | **100** |
| **Asilimia ya Uzito wa Vipengele vya Maswali kwa kila Ujuzi** | | | | | | | | | |